

WIZI WA MONSANTO WA KAROTI YA ZAMBARAU YA UTURUKI

UNYANG'ANYI DHIDI YA WAKULIMA KWA AJILI YA KUPATA FAIDA!

Wizi uliofanywa na Monsanto wa karoti ya zambarau ya Uturuki unaonyesha jinsi makampuni makubwa yanavyoiba aina za mimea za wakulima, kuwanyang'anya watu wa kawaida na kuzifanya mali yao binafsi, na baadaye warudi tena na kuwauzia wakulima wale wale aina walizowaibia!

Wizi wa hakimiliki za kibaiolojia za watu wa kawaida: kuwaibia wakulima aina zao za mbegu!

Mtu mmoja aitwaye Bw. John Wester alinunua mbegu za karoti ya zambarau katika gulio mjini Adana, Uturuki na kuzituma kwenye Kampuni ya Monsanto, Seminis. Seminis ilichofanya ni kupanda tu zile mbegu na haraka kuchagua karoti bora kwa madhumuni yao, kama vile zile ambazo zina umbo la mizizi na rangi ya zambarau zinazotakiwa. Mchakato huu rahisi wa kuchagua mbegu ulikamilika katika kipindi cha vizazi sita huko California, Marekani kati ya mwaka 2000–2004. Baada ya hapa Seminis iliomba na kupata Hakimiliki ya Kulinda Aina ya Mmea kwa aina hii ya karoti nchini Marekani na baadaye Ulaya. Hakimiliki hii iliwapa Monsanto haki ya pekee ya kuuza mbegu "yao" ya karoti ya zambarau.

Seminis wanadai kwamba walizipata mbegu hizi kihalali, kwa maana ya njia ile ile ya kukusanya mazao kutoka porini au maeneo ya mbali kwa madhumuni ya hifadhi. Lakini hii si kweli! Waliiba mbegu hii iliyoendelezwa kupitia juhudi za wakulima kwa vizazi vingi, wakadai ni ya kwao na kuiza kwa faida! Huu ni wizi wa hakimiliki za kibaiolojia.

